

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA TISA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATU

9 NOVEMBA, 2017

KIKAO CHA TATU – TAREHE 9 NOVEMBA, 2017

I. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Job Y. Ndugai (Spika wa Bunge) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

MAKATIBU MEZANI:

1. Ndg. Stephen Kagaigai
2. Ndg. Nenelwa Wankanga
3. Ndg. Lawrence Makigi

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

Mhe. Waziri Mkuu aliulizwa maswali mbalimbali kama ifuatavyo:-

- | | | |
|--------------------------------|---|---------|
| 1. Mhe. Freeman Aikael Mboge | - | KUB |
| 2. Mhe. Munde Tambwe Abdallah | - | CCM |
| 3. Mhe. Mwikwabe Mwita Waitara | - | CHADEMA |
| 4. Mhe. Abdallah Ally Mtalea | - | CUF |
| 5. Mhe. Cecilia Daniel Paresso | - | CHADEMA |

III. MASWALI YA KAWAIDA:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa kama ifuatavyo:-

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 30: Mhe. Ruth Hiyob Mollel

Nyongeza: Mhe. Ruth Hiyob Mollel
 Mhe. George Malima Lubeleje

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Swali Na. 31: Mhe. Mbaraka Kitwana Dau

Nyongeza: Mhe. Mbaraka Kitwana Dau

Swali Na. 32: Mhe. Capt. Abbas Ali Mwinyi

Nyongeza: Mhe. Capt. Abbas Ali Mwinyi
Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Swali Na. 33: Mhe. Rashid Ali Abdallah

Nyongeza: Mhe. Rashid Ali Abdallah

WIZARA YA KILIMO:

Swali Na. 34: Mhe. Fredy Atupele Mwakibete

Nyongeza: Mhe. Fredy Atupele Mwakibete

Swali Na. 35: Mhe. Jerome Dismas Bwanausi

Nyongeza: Mhe. Jerome Dismas Bwanausi

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na. 36: Mhe. Doto Mashaka Biteko

Nyongeza: Mhe. Doto Mashaka Biteko
Mhe. Ally Seif Ungando
Mhe. Salome Wycliffe Makamba

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Swali Na. 37: Mhe. Devota Mathew Minja

Nyongeza: Mhe. Devota Mathew Minja

Swali Na. 38: Mhe. Esther Michael Mmasi

Nyongeza: Mhe. Esther Michael Mmasi

IV. MATANGAZO

Wageni mbalimbali waliokuwa Ukumbini kwenye *gallery* walitambulishwa Bungeni.

V. MWONGOZO WA SPIKA

1. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda alitumia Kanuni 47 kuomba Mwongozo.

Kuhusu Mikoa inayolima Mahindi kwa wingi ambayo ni Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya, Songea, Rukwa na Katavi kuzalisha kwa wingi lakini Mahindi hayo yamekosa soko na kuliomba Bunge kujadili hoja hii ili Mwaka ujao kuepusha mfumuko wa bei wa zao hili. Aidha, alieleza na zao la tumbaku lina changamoto hiyo.

Kabla ya Kiti kutoa maamuzi Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara alisema mzungumzaji ametumia Kanuni ambayo siyo na kwamba jambo hili halijatokea Bungeni.

Kiti kiliamua kwamba suala la Mhe. Mapunda halijafata Kanuni na kushauri Kamati zote za Bunge kuwa makini kuleta hoja kama hizi ambazo ni muhimu kwa Wananchi ili Bunge izishughulikie.

2. Mhe. Goodluck Araph Mlinga alitumia Kanuni 68(7) kuomba mwongozo kuhusu kauli ya Mhe. Freeman Aikaeli Mbewe kutaka uchunguzi wa kimataifa kwa suala la Mhe. Tundu Antiphas Lissu kinyume na Katiba na kinaleta matabaka kwenye jamii kwani

matukio ya Albino, Kibiti n.k. hakuna uchunguzi wa Kimataifa uliofanyika.

Kiti kilijibu kwamba kwamba hakuna Mwongozo uliombwa.

VI. KAULI ZA MAWAZIRI:

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia alitoa kauli kuhusu Udhili na Utoaji wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa Mwaka 2017/2018.

VII. HOJA ZA SERIKALI

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali 2018/2019.

VIII. KAMATI YA MIPANGO

Bunge lilikaa kama Kamati ya Mipango na Mjadala wa Mapendekezo ya Mpango kwa Mwaka 2018/2019 uliendelea na Wabunge wafua walichangia:-

- | | | | |
|-----|-----------------------------|---|-----|
| 35. | Mhe. Peter Joseph Serukamba | - | CCM |
| 36. | Mhe. Ally Saleh Ally | - | CUF |

Taarifa

Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma alimpa Taarifa Mhe. Ally Saleh Ally kwamba mgawanyiko wa CUF haujafanywa na Nchi, CCM au Bunge bali ni Katibu Mkuu, Maalim Seif. Mhe. Ally Saleh Ally alikataa Taarifa hiyo na aliendelea kuchangia.

- | | | | |
|-----|-------------------------------|---|---------|
| 37. | Mhe. Richard Mganga Ndassa | - | CCM |
| 38. | Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa | - | CCM |
| 39. | Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi | - | CHADEMA |

Taarifa

Mhe. Goodluck Araph Mlinga alimpa Taarifa mzungumzaji akimtaka aseme Bashite ni nani katika nchi hii. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi alikataa Taarifa hii na kuendelea kuchangia.

- | | | | |
|-----|-----------------------------|---|---------|
| 40. | Mhe. Hussein Mohamed Bashe | - | CCM |
| 41. | Mhe. Jesca David Kishoa | - | CHADEMA |
| 42. | Mhe. Freeman Aikaeli Mbewe | - | CHADEMA |
| 43. | Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu | - | CCM |

IX. BUNGE KURUDIA NA KUSITISHWA

Saa 7:00 mchana Bunge lilitrudia na kusitishwa mpaka Saa 11:00 jioni.

X. BUNGE KURUDIA

Saa 11:00 jioni Bunge liliendelea na Kamati ya Mipango na wafuatao walichangia.

- | | | | |
|-----|---------------------------------|---|---------|
| 44. | Mhe. John Peter Kadutu | - | CCM |
| 45. | Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab | - | CCM |
| 46. | Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi | - | CCM |
| 47. | Mhe. Sonia Jumaa Magogo | - | CUF |
| 48. | Mhe. Almas Athuman Maige | - | CCM |
| 49. | Mhe. Edwin Mgante Sannda | - | CCM |
| 50. | Mhe. Aeshi Khalifan Hilaly | - | CCM |
| 51. | Mhe. Joseph Roman Selasini | - | CHADEMA |

Taarifa

Mhe. Gooldck Araph Mlinga alimpa Taarifa Mhe. Joseph Roman Selasini kuwa Taarifa alizomhusisha nazo za mauaji si za kweli na mzungumzaji alikataa Taarifa hiyo.

Mhe. Joseph Kasheku Musukuma alimpa tahadhari kuzungumzia mchango aliota jana lakini Mhe. alikataa na kuendelea kusisitiza Hansard yake iangaliwe na baadhi ya maneno yaondolewe kwa kuwa siyo mazuri.

- 52. Mhe. Agnes Mathew Marwa - CCM
- 53. Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula - CCM
- 54. Mhe. Omary Tebweta Mgumba - CCM
- 55. Mhe. Amina Saleh Mollel - CCM

XI. BUNGE KURUDIA NA KUAHIRISHWA

Saa 1:45 jioni Bunge lilimaliza kujadili Mapendekezo ya Kamati ya Mipango na lilirudia ambapo lilahirishwa mpaka Ijumaa tarehe 10 Novemba, 2017 saa 3:00 asubuhi.